# *Umoja wa Mungu Mmoja Katika Lile Kanisa Moja*

[Ndugu Neville anasoma mlango wa 17 wa Yohana Mtakafifu:]

[*Maneno hayo Yesu aliyasema, akainua macho yake mbinguni, akasema, Baba, saa imekwisha kufika; mtukuze Mwanao, ili Mwanao naye akutukuze wewe:*]

[*Kama vile ulivyompa mamlaka juu ya wote wenye mwili, ili kwamba wote uliompa awape uzima wa milele.*]

[*Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.*]

[*Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi uliyonipa niifanye.*]

[*Na sasa, Ee Baba, unitukuze mimi pamoja nawe kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe kabla ya ulimwengu kuwako.*]

[*Jina lako nimewadhihirishia watu wale ulionipa katika ulimwengu: walikuwa wako, ukanipa mimi; na neno lako wamelishika.*]

[*Sasa wamejua ya kuwa yote uliyonipa yatoka kwako.*]

[*Kwa kuwa maneno uliyonipa nimewapa wao, nao wakayapokea, wakajua hakika ya kuwa nalitoka kwako, wakasadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.*]

[*Mimi nawaombea hao: siuombei ulimwengu, bali hao ulionipa; kwa maana hao ni wako.*]

[*Na wote walio wangu ni wako, na walio wako ni wangu; nami nimetukuzwa ndani yao.*]

[*Wala mimi simo tena ulimwenguni, lakini hawa wamo ulimwenguni, nami naja kwako. Baba Mtakatifu, kwa jina lako mwenyewe uwalinde hawa ulionipa, ili wawe na umoja kama sisi tulivyo.*]

[*Nilipokuwa pamoja nao ulimwenguni, mimi niliwalinda kwa jina lako: wale ulionipa nimewatunza, wala hapana mmojawapo aliyepotea, ila yule mwana wa upotevu; ili andiko litimie.*]

[*Na sasa naja kwako, na maneno haya nayanena ulimwenguni, ili wawe na furaha yangu imetimizwa ndani yao.*]

[*Mimi nimewapa neno lako; na ulimwengu umewachukia, kwa kuwa wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu.*]

[*Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu, bali uwalinde na yule mwovu.*]

[*Wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu.*]

[*Uwatakase kwa ile kweli: neno lako ndiyo kweli.*]

[*Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo nimewatuma hao ulimwenguni.*]

[*Na kwa ajili yao najiweka wakfu mwenyewe, ili wao pia watakaswe katika ile kweli.*]

[*Wala si hao tu ninaowaombea, lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao;*]

[*Ili wote wawe kitu kimoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako, hao nao wawe ndani yetu: ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.*]

[*Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe kitu kimoja, kama sisi tulivyo kitu kimoja:*]

[*Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa wewe ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi.*]

[*Baba, hao ulionipa nataka wawe pamoja nami po pote nilipo; wapate na kuutazama utukufu wangu ulionipa: kwa maana ulinipenda kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.*]

[*Ee Baba mwenye haki, ulimwengu haukukujua: lakini mimi nimekujua, na hawa wamejua ya kuwa ndiwe uliyenituma.*]

[*Nami nimewajulisha jina lako, tena nitawajulisha hilo: ili pendo lile ulilonipenda mimi liwe ndani yao, nami niwe ndani yao.*]

2 [“Na Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa mlango mzima, mlango wa 17 wa Injili ya Yohana Mtakatifu.”—Mh.]

3 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Asante, Ndugu Neville. [Ndugu Neville anasema, “Mungu akubariki, Ndugu Branham.”] Bwana akubariki, Ndugu Neville.

4 Mimi ni kama tu Ndugu Neville, nina ninii. . . sikuweza tu kungoja hadi Krismasi, kufungua zawadi hiyo. Na, mnajua, mara moja mtu mzima na mara mbili mtoto. Kama. . . Lakini bila shaka nafikiri Ndugu Neville anaonekana mzuri sana katika suti yake mpya.

5 Nami nilipata moja ya makoti mazuri sana niliyowahi kuona maishani mwangu, kutoka kwa kanisa hili hapa chini, na bila shaka ninalithamini. Nawashukuru kwa kunichukua kuwa mkubwa kidogo kuliko vile nilivyo, lakini naamini wataniletea moja lililo dogo kidogo tu, kesho. Kidogo ni koti kubwa sana kwa mtu mzima ambaye linapaswa kumfunika. Kwa hiyo mlisikia, katika Biblia, ambapo blanketi ilikuwa fupi mno kwa mtu huyo, ama kitanda; kwa hiyo ni karibu tu hivyo kwa—kwa hili hapa nililo nalo, kwa sababu hi—hilo koti lilikuwa kubwa kidogo tu. Lakini bila shaka ni zuri, na ninatumaini wanalo moja kule yapata namba moja kidogo zaidi, ambalo litanienea vizuri sana. Nami nitalichakaza, pia, ili kulionyesha kama alivyofanya kule.

6 Nimeona wakati ambapo nimehubiri nikiwa nimevaa koti, vema, nikifurahia kulivaa. Vema, sijapata koti zuri maishani mwangu mwote. Hii ni mara yangu ya kwanza kuwahi kumiliki koti zuri.

7 Ninashangaa tu kama kanisa hili linaweza kukumbuka kuondoka kwangu kwa mara ya kwanza kutoka humu kanisani. Mnakumbuka ilivyokuwa usiku ule nilipoenda St. Louis, kutoka kanisa hili, kumtembelea binti ya Robert Daugherty? Sasa, Dada na Ndugu Spencer, nadhani, wanaweza kukumbuka. Ndugu Roy Slaughter hapa, wengi wao ambao. . . Hata sikuwa na koti lolote kamwe. Na kanisa likachangia dola kumi na moja kwa tikiti yangu. Kisha nikaazima koti la ndugu yangu. Nalo lilikuwa kubwa karibu maradufu kwangu, ndipo ikanibidi kulibeba kwa sababu ilionekana baya sana kwangu kulivaa. Na halafu nilionekana vibaya kutokuwa na lolote, kwa hivyo ni—nikalibeba. Basi nilipofika kule, nilikuwa huko siku kadhaa, naye Bwana akaanza kutenda kazi, na kumponya mtoto Betty.

8 Unajua, nilimwona si muda mrefu uliopita, yeye ni mwanamke kijana mzuri sasa. Alikuwa na ugonjwa wa ngoma ya Mtakatifu Vitasi, na alikuwa amelala tu kama mnyama, akijikwatua-kwatua, kwa siku kadha wa kadha. Nao madaktari walio bora sana walikuwa wamemkatia tamaa. Nilikaa siku hiyo na jioni hiyo. Bwana alionyesha ono tu juu ya nini cha kufanya, na kusema, "Mtoto Betty atakombolewa mara tu watakapofanya hivyo."

9 Nikamwambia huyo mhudumu pamoja na baba yake wasimame. Nikamwambia huyo mama, "Ulikuwa mjini hivi majuzi, ukinunua sufuria ndogo, na ukanunua moja ambayo ni sufuria ya itale ya bluu. Iko kwenye makabati yako, humo chini. Hujawahi kuisogeza tangu ulipoiweka humo."

10 Akaanza, akasema, "Hiyo ni kweli."

11 Nikasema, "Nenda ukaichukue na kuijaza maji, kisha ulete taulo ndogo nyeupe, uje hapa. Kwa maana, BWANA ASEMA HIVI, mtoto Betty ataponywa." Na . . .

12 [Ndugu Roy Slaughter, anasema, "Ndugu Branham, ningependa tu kusema neno moja, ikiwa ni sawa?"] Naam, endelea. ["Unajua ulipokuwa huko nje, unakumbuka kwamba—kwamba nilikupigia simu. Msichana wetu alikuwa mgonjwa. Nawe ukampigia simu mkeo, na kumwambia. Vema, mwanzoni, nilikupigia simu, na kuacha ujumbe, 'Tayari, madaktari watano walisema hakukuwa na matumaini kwa wataalamu wa matibabu."] Naam. ["Ndipo ulipoingia, ulisema, 'Kuna simu kutoka kwa Ndugu Slaughter, utaipokea . . .?' Nawe ulisema, 'Huyo ni mmoja wa marafiki bora sana nilio nao,' ama kitu kama hicho."] Naam, bwana. ["Nawe ukaenda ukaomba. Ulienda ukamwita mkeo, ukasema atupigie simu na kuwaambia, 'Msichana atakuwa mzima.' Naye hakujua alikuwa mgonjwa, unaona."] Naam. ["Na—na kwa hiyo, akaenda kesho yake, naye alikuwa hospitalini. Madaktari wakaingia. Wakasema, 'Kitu fulani kime—kimetukia . . . kilifanyika.' Anasema, 'Naam.' Nao kidogo wakaanza kupitia, labda, yale waliyokuwa wamefanya. Akasema, 'Hapana.' Akasema, 'Ilikuwa ni maombi ya Ndugu Branham.'"] Naam, nakumbuka hilo. ["Alikuwa na homa, hata hawakujua shida ilikuwa nini, kulikuwa na madaktari watano, kwa hiyo . . . kwenye wakati huu. Lakini nilipokuja, nilikuja kutoka hudumani, kukupigia simu; naye mke alikuwa akituma mtoto kwangu, nikupigie simu. Alikuwa ametoka huko nje, 'Kumpigia simu Ndugu Branham.'"] Naam. ["Kwa hiyo, ilikuwa ni kwa bahati tu, tulikutana hudumani. Ndipo nilipokupigia simu, basi ukaomba. Nawe ukapiga simu tena, ukasema, 'Mwambie, msichana huyo ni sawa.' Naye yuko sawa."] Naam.

13 Mpenzi, nadhani unakumbuka hilo, sivyo, tulipokuwa huko St. Louis, kwenye—kwenye mkutano, ambapo msichana mdogo wa Ndugu Slaughter aliugua sana. Nasi tulikuwa kwenye Hoteli ya kale ya Belcher Bath. Naweza kukumbuka hilo vizuri tu! Nasi tukachukua ujumbe, na kwenda mbele za Bwana, Naye akaonyesha ono, akasema. Ndipo nikampigia simu Ndugu Slaughter na hao wengine, nikawapigia simu na kusema, "Waambie, 'BWANA ASEMA HIVI. Usijali, ataishi.'" Naye akaishi. Bwana alikuwa mwema sana!

14 Kumekuwako na mambo mengi yametokea tangu wakati huo, lakini Yeye angali ni Bwana Yesu yeye yule, sivyo? Ajabu sana! Siwezi kufikiria chochote bora kuliko kujua hilo. Kwamba, ikiwa ningerithi kila senti ya pesa inayomilikiwa na ulimwengu, na niwe nitaishi kwa muda wa miaka elfu moja hapa duniani, afadhali nijue nilicho nacho sasa hivi, Uzima wa Milele. Uzima udumuo utaisha baada ya muda fulani. Uzima wa Milele

hauna mwisho, kwa sababu haukuwa na mwanzo, na kwa hiyo tunashukuru kwa hilo.

15 Ndugu Neville alikuwa ndiyo kwanza asome Maandiko fulani, ambayo aliyasoma kwa niaba yangu, kutoka katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu. Na kulikuwa na Andiko moja pale, kifungu cha 21, ningetaka kuitisha usikivu wenu Kwalo, kwa muda kidogo tu. Yesu, katika maombi yake, aliomba hivi.

> *Kwamba wote wawe kitu kimoja; kama wewe, Baba,* ulivyo *ndani yangu, nami ndani yako, hao nao wawe ndani yetu: ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba ndiwe uliyenituma.*

16 Na kama nikiliita somo, ningependa kusema hivi: *Umoja wa Mungu Mmoja Katika Lile Kanisa Moja*.

17 Mnajua, Mungu amemwumba mwanadamu apate ku—kufanikisha. Hilo ndilo mwanadamu aliloumbiwa. Na kote katika maisha, amejaribu kufanikisha kitu fulani. Na mafanikio yake, sababu ya yeye kujaribu hivyo, ni kwa sababu alikusudiwa kufanya hivyo. Mungu alimwumba hivyo. Lakini shida yake ni kwamba, katika mafanikio yake, anajaribu kufanya kitu kwa nafsi yake mwenyewe. Hapo ndipo anapokosea kisha anapata matatizo.

18 Sasa, hapo mwanzo, Mwanzo, ambayo ni sura ya mbegu ya Biblia, tunaona mle ndani ya kwamba Mungu alipomwumba mtu, alimwumba jinsi alivyojua ya kuwa angekuwa. Wala asingeweza kuwa na muundo wowote mkuu zaidi kuliko vile alivyo. Alipoanza kufanya uhai, aliufanya kutoka kwa uhai wa chini kabisa, ambao ni, takriban, kiluwiluwi, chura; hadi kwenye uhai wa juu zaidi, ni mwanadamu, ambaye yuko katika sura ya Mungu.

19 Ndipo basi, katika maisha haya, mwanadamu akaanza kufanikisha mambo. Lakini, alipofanya hivyo, alianza kumwacha Mungu nje. Akaanza kuwa na nia za ubinafsi. Na—na alipofanya hivyo, akaanza kujiwazia mwenyewe jambo fulani. Nasi tunaona kwamba haikuchukua muda mrefu mpaka akawa ameichafua sayari yenyewe ambayo Mungu alikuwa amemweka juu yake. Alikuwa amefikia hali mbaya sana mpaka hata Muumba Wake akahuzunika, Yeye moyoni Mwake, kwamba kamwe alikuwa amemwumba mwanadamu. Nawe unaweza kuwazia jinsi Mungu alivyohisi alipoona kiumbe kile kile alichoumba kwa mfano Wake, na kumpa mamlaka, na jinsi ambavyo alimwumba amfanyie jambo fulani, na hata hivyo akageuza nguvu zake zote na uwezo wake kwa tamaa na mafanikio ya ubinafsi.

20 Na kisha tunaona, si muda mrefu sana baada ya somo hili kuu ambalo Mungu alimfundisha huyo mtu wakati huo, kwa kuuangamiza ulimwengu mzima kwa maji; kama vile Biblia inavyotuambia kwamba aliigharikisha dunia, na kuangamiza

kila kitu isipokuwa mabaki ambayo Yeye aliyaacha, ambayo yalikuwa ni Nuhu na familia yake. Na mara tu baada ya yeye kutoka kwenye somo hilo kuu . . .

21 Inaonekana tu kana kwamba mwanadamu hawezi kujifunza, ila tu kupitia njia ngumu. Tunaona kwamba hata kwa watoto wetu; inabidi tuwaadhibu, mara nyingi, vikali, ili kuwafanya waelewe. Inaonekana tu kana kwamba mwanadamu, ndani yake mwenyewe, ameshindwa kabisa, kwa kuanzia. Alipopoteza uhusiano wake na Mungu, akawa kitengo chake mwenyewe, hakumtegemea Mungu tena. Na Mungu alipomfundisha somo la jinsi ilivyokuwa kujaribu kufanya kitu ndani yake mwenyewe, kwamba kazi zake zote zingebatilika, mara tunawapata tena wakishuka moja kwa moja kwenda kufanikisha tena. Nayo Biblia ilisema kwamba, "Walijijengea mnara, nao walikuwa wapande waingie juu mbinguni," kupanda kwenda Mbinguni bila kupitia njia ambayo Mungu alikuwa amewapangia kupitia.

22 Naye mwanadamu anaweza kufanikiwa vizuri zaidi wakati wameungana pamoja. Sasa ukimchukua mtu mmoja, peke yake, nguvu zake zina kikomo cha mtu mmoja. Watu wawili humfanya kuwa mara mbili ya nguvu zake. Watu wanne humfanya kuwa na mara nne ya nguvu zake. Naye Mungu anatutaka tuwe kitu kimoja. Mungu alimwumba mwanadamu ili tuwe kitu kimoja, na nia zetu ziwe moja, na malengo yetu yanapaswa kuwa mamoja, na ma—mafanikio yetu yanapaswa kuwa mamoja. Ameundwa tu hivyo.

23 Basi tunaona, ya kwamba mara baada ya maangamizi yaliyotangulia ile gharika, kwamba mwanadamu alianza kujaribu kujichukulia mamlaka tena, yeye mwenyewe.

24 Na wakati wote mambo haya yanapoendelea, Roho wa Mungu aliye hai anashindana na mwili, akijaribu kumtoa mwanadamu kutoka katika mafanikio yake mwenyewe, akijaribu kumwondosha mwanadamu kutoka kwa nia na malengo yake ya ubinafsi, kumwelekeza kwenye mpango ambao Mungu ameweka. Na maadamu mwanadamu anafanya kazi kwa mpango wake mwenyewe, atakuwa ni mshindwa. Naye mwanadamu anaweza tu kufanikiwa vyema anaporudi na lengo sahihi na nia sahihi, na, yaani, sawasawa na mpango wa Mungu kwa ajili yake. Msingi mwingine wowote upo kwenye mchanga udidimiao.

25 Nasi tunaona, basi, ya kwamba wamejaribu kuungana, nao wameanza . . . kufanyika mtu mmoja. Lakini katika muungano huu waliofanikisha wakati huo, ulikuwa chini ya mamlaka ya kisiasa. Mwanadamu akawa mmoja, lengo lao lilikuwa moja, mafanikio yao yalikuwa mamoja, bali ulikuwa ni *umoja* haramu, kwa sababu ulikuwa ni kinyume na mpango wa Mungu. Lakini akazidi kuendelea.

26 Na hatimaye unapoona umoja wa namna hiyo miongoni mwa watu kama hao, wanafanya mambo makuu. Angalia tu ulimwengu leo, wakati watu wanapojiunganisha pamoja, ingawa ni chini ya mpango haramu, watafanya mambo makuu.

27 Sasa, walijenga mnara ambao natilia shaka kama sayansi ya kisasa inaweza kujenga siku hizi, pamoja na mitambo yao yote na kadhalika, kwa sababu walikuwa wameungana pamoja. Walikuwa na nia moja, nafsi moja, kusudi moja, nia moja, lengo moja, hiyo ni kusema, "Kujenga mnara mrefu sana ambao kama Mungu angewazia kuwaangamiza, tena, wangepanda mbio moja kwa moja hata mbinguni pamoja Naye. Wala kusingekuwa na njia ambayo wangeweza kumzuia asiwaangamize, ama Yeye angewazuia kuujenga," kama walivyodhania. Nasi tunaona, basi, ya kwamba walikuwa wamejipanga pamoja, na tunawapata tena nje kabisa ya mapenzi ya Mungu.

28 Na ikiwa hiyo siyo picha nzuri ya siku hizi, ambapo watu wanajaribu kuungana pamoja! Nasi tunapaswa kuungana, lakini wanaungana chini ya mifumo haramu. Je, umewahi kuona jinsi ibilisi anavyoyaiga mambo ya Mungu? Je, umewahi kuona jinsi anavyochukua mambo ambayo Mungu amekusudia?

29 Na jambo baya ni danganyifu sana! Sasa, uwongo, ukiwa moja kwa moja kutokana na uwongo halisi, basi mtu yeyote anaweza kuugundua. Lakini uongo huo ulio na ukweli takriban asilimia tisini na tisa ndani yake, huo ndio unaodanganya.

30 Je, umeona jinsi ambavyo ibilisi alimdanganya Hawa? Kila kitu alichomwambia kilikuwa ni ukweli mtupu, ila jambo moja. Kasema, "Macho yako yatafumbuliwa, nawe utajua mema na mabaya, na—na kadhalika. Nanyi mtakuwa kama miungu, kwa sababu hamjui mema na mabaya sasa." Na mambo hayo yote yalikuwa ni kweli.

Lakini wakati aliposema, "Bwana Mungu alisema 'tutakufa.'"

31 Alisema, "Hakika hamtakufa." Mnaona, kiasi fulani tu cha Ukweli ndani yake, halafu kiasi kidogo tu cha uongo.

32 Naye Yesu alisema, duniani, "Chachu kidogo huchachua donge zima." Na haina budi kuwa kweli kabisa, ama si kweli hata kidogo. Nao mpango wa wokovu hauna budi kuwa sahihi, na ahadi za Mungu ni kamili, nazo hufanya kazi kikamilifu, la sivyo kuna—kuna kasoro mahali fulani. Na ikiwa Kanisa la Mungu aliye hai halifanikishi kile ambacho Mungu alikusudia wafanye, kuna kasoro katika mfumo huo, mahali fulani. Hapana shaka!

33 Hebu chukua kipande kizuri cha mtambo, kama saa, na hebu kila kipande cha mtambo huo kifanye kazi kwa upatanifu, nayo itadumisha wakati kikamilifu. Lakini wakati kipande kimoja kinapoenda njia moja, na kimoja njia nyingine, haitadumisha

wakati. Haijalishi vito ni vizuri jinsi gani, vyote havina budi kuunganishwa pamoja.

Na hilo ndilo kusudi la Mungu, kwetu kuungana pamoja na kuwa kitu mmoja.

34 Lakini tunaona hapo, ya kwamba, jinsi ibilisi anavyoiga vitu. Udhalimu wote ni uadilifu tu uliopotoshwa. Uongo ni ukweli tu uliogeuzwa. Mambo mazuri ambayo Mungu hufanya; mambo mabaya ni mambo mazuri yaliyopotoshwa. Hivyo basi, kwamba, udhalimu ni haki iliyopotoshwa. Shetani hawezi kuumba chochote, mwenyewe. Inambidi tu kuchukua kile ambacho Mungu ameumba, kukipotosha. Mwanamume anayeishi na mkewe, yuko sawa kabisa; lakini kumchukua mwanamke mwingine, hicho ni kitendo kile kile, kimepotoshwa, na ni mauti. Kimoja huleta uzima, kingine huleta mauti. Hiyo ndiyo njia, ambayo, ma—mambo yote ambayo Shetani anaweza kuyafikia, ni kuchukua tu kile ambacho Mungu ameumba, na kukibadilisha.

35 Je, umewahi kuwazia kuhusu dini ya Muhammad? Kwenye kaburi la Muhammad, kumekuwa na farasi mweupe aliyetandikwa kwa miaka elfu mbili. Kila baada ya saa nne, mlinzi anabadilishwa na farasi mwingine mweupe analetwa. Nao wanafanya hivyo kwa uchaji, pamoja na imani thabiti kwamba Muhammad atafufuka siku moja na kuuteka ulimwengu. Wanaliamini. Basi umewahi kufikiria kwa nini farasi mweupe? Je, unajua Maandiko yanasema, kwamba, "Yesu atakuja, amepanda farasi mweupe, na vazi Lake lililochovywa katika damu, na Jina Lake aitwa Neno la Mungu"? Ni Bwana Yesu, atakuja, akipitia mbinguni, pamoja na majeshi nyuma Yake, wamepanda farasi mweupe. Je, unaweza kuona hiyo dini potovu, waligeuka na kuifanya ati Muhammad a—amepanda farasi mweupe? Lakini, Yesu anakuja mbinguni; naye Muhammad ni wa duniani. Kwa hiyo, Shetani anafanya kazi na kitu cha duniani, wakati Mungu anapofanya kazi na mbingu.

36 Pia mliwahi kuwazia juu ya mnara wa Babeli na kuulinganisha na ngazi ya Yakobo? Jinsi walivyokuwa wakijaribu kujenga vipandio kuzunguka mnara ambao ungefika Mbinguni, wakijaribu tu kuipotosha ngazi ya Yakobo iliyotoka mbinguni ikashuka duniani na Malaika wakishuka na kupanda. Kuipotosha!

37 Uliwahi kuwazia juu ya U.N. sasa wakijaribu kuyafanya mataifa yote, udugu mmoja mkubwa, chini ya mamlaka yaliyounganishwa? Kuungana, ni sawa, lakini kuko chini ya kitu kibaya. Shetani anatawala mataifa yote. Maandiko yanasema kwamba Shetani ndiye mtawala wa dunia. Alipompeleka Yesu juu ya mlima mrefu sana, akamwonyesha falme zote za duniani, na kusema, "hizi ni zangu." Yesu hakusema hazikuwa. Kwa

maana, ni zake. Hiyo ndiyo sababu tuna vita na mauaji, ni kwa sababu kwamba falme hizi za ulimwengu zinatawaliwa na ibilisi. Na maadamu zinatawaliwa na ibilisi, tutaendelea kuwa na vita na kushambuliana, na kuuana.

38 Lakini tunautazamia Ufalme ujao, ambapo Kristo atakuja, wala hakutakuwako na vita tena. Na kutakuwa na amani ya milele.

39 Je, uliwazia ya kwamba, katika Urusi hii, wanayo Pentekoste ya uongo? Wao ni. . .Hiyo ni kazi ya ibilisi. Wanajaribu kuwalazimisha watu wote kuingia katika ukomunisti, ambapo kila mtu ana kila kitu shirika. Je, mnajua hiyo ndiyo iliyokuwa hali ya Kanisa chini ya Roho Mtakatifu, kwenye Siku ya Pentekoste? kwamba watu waliuza mali zao na kuziweka miguuni pa wanafunzi, nao wakawagawia kila mtu kadiri walivyohitaji. Na sasa ibilisi amerudi, na kuingia ulimwenguni na kutengeneza mamlaka ya kisiasa, kumlazimisha mwanadamu kwa jambo hilo.

40 Mungu hamlazimishi mwanadamu kufanya lolote. Unafanya kwa hiari yako mwenyewe. Anaweza kukuonya, atupe kizuizi katika njia yako. Bali unatembea kwa nafsi yako mwenyewe, kwa uamuzi wako mwenyewe, katika Uwepo Wake, kumfanya Yeye Mwokozi wako. Lakini Shetani ameipotosha mipango ya Mungu, ikawa ni mpango wake mwenyewe.

41 Je, uliwahi kuwazia juu ya Ukatoliki, na kanisa Katoliki linajaribu kumfanya kila mtu kuwa Mkatoliki? Haitafaulu. Iko chini ya mpango wa kujibunia.

42 Uliwahi kuwazia juu ya kanisa la Kiprotestanti chini ya muungano wa makanisa, linajaribu kuyaondosha makanisa haya yote madogo? Na litatukia, kwamba hutaweza kwenda kanisani isipokuwa uwe mfuasi wa muungano wa makanisa, ndipo sehemu ndogo ndogo kama hizi hakika zitabeba gharama yake. Lakini tuna Maandiko yanayosema, “Msiogope, enyi kundi dogo, Baba yenu ameona vema kuwapa ninyi ule Ufalme.” Huo ndio tunaotarajia.

43 Halafu, unaona, yote ni mafanikio ya adui anayojaribu kufanya, kufanikisha, lakini chini ya mpango haramu. Ni chini ya mpango wake mwenyewe, lakini hana wa asili. Yeye hana budi kuchukua jambo ambalo Mungu amefanya, kisha kulipotosha liwe udhalimu, kulifanya.

44 Leo wanajaribu kuupotosha ulimwengu, au kuugeuza kuwa muungano mmoja mkubwa sana wa—wa mataifa, udugu. Na kama ungekuwa chini ya uigaji wa kujibunia, ungekuwa na kiongozi, naye angekuwa ibilisi kwa sababu yeye ndiye kiongozi wao wote.

45 Ufalme wa Mungu si wa dunia hii. Ufalme wa Mungu uko mioyoni mwetu. Ni Ufalme wa kiroho, ambao tunazaliwa ndani Yake. Yesu alisema, “Ufalme wa Mungu huja, bali sio

bila kutumia nguvu. Nao Ufalme wa Mungu uko ndani yenu." Roho Mtakatifu, Ufalme wa Mungu, akitenda kazi ndani ya mwanadamu, na kumwogoza na kumtawala, huo ndio Ufalme.

46 Nasi tunaona ya kwamba mataifa haya yanazunguka-zunguka, yakidanganyana, yakizungumza amani; wakiwa na kisu nyuma yao, tayari tu kuangamizana.

47 Siku chache zilizopita, nilipata fursa ya kuzungumza na kasisi ambaye ni mtu mashuhuri. Basi, huko California, walikuwa na wanasayansi, baadhi ya walio bora sana tulio nao katika mataifa, walikuwa wamekutana huko kwa ajili ya mkutano, na ku—kuwa na mkutano wa siri, usioruhusiwa watu wengine. Na kwa kuwa hali ilikuwa ya kutisha sana, walimwalika kasisi wa jeshi awe pamoja nao. Na huyu kasisi rafiki yangu, akasema, "Ndugu Branham, kabla sijaweza kuingizwa ndani, waliipekua kumbukumbu yangu, hata kifikia mama wa nyanya yangu, kabla sijaingia kwenye mkutano huu." Naye akasema, "Laiti nisingekuwa humo." Akasema, "Wanasayansi hao walipoinuka na kuanza kuzungumza," akasema, "ilionekana ukungu ulishuka humo chumbani, uliokufanya uhisi kama ulikuwa kwenye nyumba ya barafu, baridi, jinsi ingeigandisha damu ya mtu!" Kasema, "Wao, haturuhusiwi kuzungumza juu ya mambo haya. Tumeapishwa chini ya kiapo."

48 Lakini akasema, "Nimeruhusiwa kuwaambia *hivi*." Akasema, "Wanajiandaa kuachana na jeshi na pamoja na wa angani, jeshi la angani, na kadhalika." Kasema, "Hawawahitaji tena." Akasema, "Wana silaha hatari sana hivi kwamba wanaweza kuiangamiza dunia nzima kwa sekunde moja." Kisha akasema, "Kama wangeacha hilo lijulikane, hilo, watu wangeingiwa na hofu kuu, kisha waende mitaani, wakipiga mayowe kwa nguvu zao zote." Kasema, "Wanalo bomu ambalo likianguka duniani, bomu moja tu lingelipua maili mia moja na sabini na tano pande zote, na kina cha zaidi ya futi mia moja."

49 Ungeweza kwenda kujificha wapi? Vipi kama ulijichimbia futi elfu moja? Usingeweza; ungeingia kwenye mlipuko wa volkeno ya dunia. Lakini kama ungeweza kuchimba futi elfu moja chini ya ardhi, mtikiso kama huo ukigonga juu yako, ungekuponda ukawa unga.

50 Kasema, "Mwanasayansi huyu mashuhuri akasimama, naye alikuwa mwanasayansi hodari wa jeshi. Akasema, 'Waungwana, laiti ningalimchukua maskini ng'ombe mzee pamoja na mkokoteni, niende nyuma ya milima, na kusahau yote kuyahusu, na niutumikishe wakati wangu mdogo duniani, kisha niondoke.' Akasema, 'Lakini tunapaswa kukabiliana nayo. Kuenda nyuma ya mlima hakutasaidia chochote.' Kasema, 'Milima hiyo ingekuwa unga mtupu, au majivu ya volkeno.'"

51 Loo, ndugu, inafaa kujua ulipo na mahali pa kutorokea, katika wakati huo! Tuna mahali pa kutorokea. Tuna kimbilio. Kimbilio hilo liko chini ya mbawa za ulinzi wa milele wa Bwana; ukijua haya, ya kuwa mnayo nafsi isiyoweza kufa, ambayo haikuumbwa kwa atomi, au kwa haidrojeni, au kwa oksijeni, au kwa chochote kilicho juu ya dunia hii; imeumbwa kwa Roho, ambayo Mungu Mwenyezi aliumba, Mwenyewe, na kukupa wewe.

52 Ni siku ya jinsi gani tunayoishi, ni wakati wa jinsi gani, kwamba pale ambapo mwanadamu amefanikisha na amefanikisha mpaka amefanikisha mambo haya mwenyewe. Sasa atafanya nini nayo?

53 Mnaona, Shetani hutumia kichwa cha mwanadamu. Alichagua hicho katika bustani ya Edeni, kuchukua kichwa cha mwanadamu, mawazo yake. Naye amelishusha hilo hata kanisani. Mnaona, ibilisi huchukua kichwa cha mwanadamu, ili aweze kutumia jicho lake. Na kama utaangalia, kama mtu huyo hajazaliwa mara ya pili kwa kweli, kiroho, atachukua kile anachoweza kuona kwa macho yake, kiburi cha maisha. Naye ataenda, watu wengi, kusema ata—atafanikisha jambo fulani, anataka kujiunga na kanisa. Anataka kuwa wa kidini. Naye atatafuta kote mpaka anapoweza kupata kanisa kubwa zaidi analoweza kupata, kwa maana mwanadamu anataka kufanya jambo kubwa. Anataka kujitengenezea jina kubwa. Hivyo ndivyo mtu wa kimwili, mpumbavu anavyowazia, "Loo, laiti ningeweza kuwa na dhehebu langu! Laiti ningeweza kuongeza maelfu kadhaa kwenye dhehebu langu, basi litakuwa kubwa kuliko yote nchini, la aina yake!" Hilo lina faida gani? Lakini anadhani anafanikisha kitu kwa sababu anawaongeza wengi zaidi.

54 Ninaamini ilikuwa miaka kadhaa iliyopita, katika 1944, ambapo Wabaptisti walitoa msemo, "Milioni moja zaidi katika mwaka wa '44." Na walipata nini walipopata milioni moja zaidi? Kama vile tu kujiunga na chama, kama hawakuwa wanafunzi halisi wa Kristo waliozaliwa mara ya pili. Walikuwa tu Wabaptisti kwa jina.

55 Angalieni madhehebu hayo mengine, la Kilutheri, Presbiteri, Wapentekoste, madhehebu mengine yote, ni yale yale. Wanajaribu kufanikisha jambo fulani. Wanataka kufanya jambo kubwa, mnaona, kwa maana analitazama jicho lake. Anawaza kwa jicho lake. Na mara nyingi haelewi ya kwamba hilo ndilo jambo ambalo hapaswi kufanya. Lakini, ibilisi huchukua jicho la huyo mtu, anamwonyesha kitu kizuri. Anayafunga macho yake kukitazama. Naye ameliingiza hilo kanisani, katika mawazo ya kiakili ya mwanadamu.

56 Siku moja, mwinjilisti huyu mashuhuri, Billy Graham, alisimama hapa Louisville, na kuinua Biblia yake. Akasema,

"*Hiki* ndicho kiwango cha Mungu." Naye yuko sahihi. Yuko sahihi kabisa. Mordekai Ham, mwinjilisti, (makao yangu ya zamani ya Kentucky), pamoja na mimi, tulikuwa tumeketi kwenye meza moja; ambapo, Billy aliongoka chini ya Mordekai Ham. Nasi tulikuwa tumeketi pale. Naye akasema, "Inakuwaje?" Akasema, "Paulo alikwenda katika mji mmoja na kupata mwongofu mmoja, akarudi mwaka mmoja baadaye naye alikuwa na thelathini kwa huyo mmoja." Kasema, "Mimi naenda kwenye mji na kupata waongofu elfu ishirini, narudi katika mwaka mmoja wala siwezi kupata ishirini. Kuna kasoro." Ndipo akasema, "Mnajua ni nini? Ni nyinyi wahubiri wavivu mnaokaa kwenye majengo, ofisi zenu, huku mmeweka miguu juu ya dawati, wala hamwendi kuwatembelea hao watu."

57 Nikawazia, "Billy, hilo ni jambo zuri sana kiakili. . . " tafadhalini msininukuu, "lakini sivyo ilivyo." Ni wachungaji gani waliomwendea huyo ambaye Paulo alimwongoa?

58 Haikuwa hivyo. Liko hapa. Hiyo inayoitwa mikutano siku hizi, nayo ni mikutano mikuu kweli, ila inafanya kazi tu kwa sehemu ya kiakili ya mwanadamu. Mtu anaingia chini ya mpagao wa uamsho, naye anasema, "Naam, namkubali Kristo," naye anamkubali kiakili kwa sababu yuko katika umati mkubwa. Anafanya hivyo kwa sababu kuna wahudumu mashuhuri mbele yake, lakini ni dhana tu ya kiakili. Mtu huyo hawezi kamwe kuendelea mbele. Hana budi kutoka akilini mwake, hadi moyoni mwake, na kuzaliwa mara ya pili, la sivyo hataweza kamwe kustahimili jaribio.

59 Dhana ya kiakili ni sawa, lakini wakati. . .Kumbukeni, jicho linapoitazama, ibilisi hulitumia jicho lako. Katika bustani ya Edeni, ilithibitika kwamba ibilisi alichagua kichwa cha mwanadamu, kufanya kazi ndani yake, lakini Mungu huchagua moyo wake. Ibilisi humwonyesha, kwa macho yake, kitu ambacho anaweza kuona, na anasema, "Kuona ni kuamini."

60 Lakini Mungu anapomjia mwanadamu, Yeye huja moyoni mwake. Naye anamjalia kuamini mambo kwa moyo wake, kwa imani, ambayo macho yake hayaoni. Kwa maana Maandiko yanasema, kwamba, "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana."

61 Mungu akitenda kazi *hapa*; Shetani akifanya kazi *hapa*. Kwa hivyo shule hizi kubwa na seminari zina faida gani kwa vyovyote vile? Wakati mwingine, sio siku zote, lakini mara nyingi sana, inavuta kutoka *hapa*, hadi *hapa*; wakati inapopaswa kuchukuliwa kutoka *hapa*, hadi *hapa* chini katika moyo wa huyo mwanadamu.

62 Mnajua, Maandiko yanasema, "Aonavyo mtu moyoni mwake, ndivyo alivyo."

63 Kafiri wa kale na mkosoaji walikuwa wakisema, "Jinsi Mungu alivyokuwa mpumbavu, kusema kwamba kulikuwa na

uwezo wa kiakili ndani ya moyo wa mtu, kwa maana hamna kituo hapo cha kuwazia."

64 Lakini yapata miaka minne iliyopita, sayansi iligundua kwamba ndani ya moyo wa mwanadamu kuna uwezo wa kufikiria. Kuna chumba kidogo, mahali padogo ambapo hakuna hata seli; chumba kidogo katika moyo wa mwanadamu. Hakipo katika mnyama au kiumbe hai mwingine yeyote. Lakini ndani ya moyo wa mwanadamu kuna mahali padogo, na hawakuweza kufikia uamuzi kwamba ni nini, lakini hatimaye wakasema hivi, "Ni mahali ambapo nafsi inakaa."

65 Kwa hiyo Mungu hunena maneno Yake kwa usahihi, "Aonavyo mtu moyoni mwake, ndivyo alivyo." Sio kichwani mwake! Ikiwa Mungu angemaanisha *kichwa*, angesema, "kichwa." Alisema, "moyoni mwake."

66 Vipi kama, Musa, alipopanda, naye Musa...Mungu akasema, "Vua viatu vyako, Musa, uko mahali patakatifu." Vipi kama Musa angesema, "Sasa ngoja kidogo, Bwana, najua ulimaanisha *kofia* yangu. Nitavua tu kofia yangu, hiyo ina heshima zaidi"? Hakusema *kofia*, alisema "viatu"! Hivyo ndivyo Yeye alivyomaanisha.

67 Hakumaanisha kamwe kupeana mikono na kujiunga na kanisa. Alisema, "Lazima uzaliwe mara ya pili, na huko ni kutoka Juu." Sio kuweka jina lako kwenye kitabu; bali uzaliwe upya, na nafsi yako ibadilishwe, utu wako wote upate kufanywa upya tena.

68 Sasa, wakati mtu ha—hajawahi kupata tukio hilo, yeye bado ni mwana wa Mungu, katika uumbaji, mwana wa Mungu aliyeanguka. Hiyo ndiyo sababu anaweza kuchukua mbao na kutengeneza majengo, anaweza kuchukua chuma na kutengeneza mtambo, anaweza kuchukua vito na kutengeneza saa. Anaweza kufanya nini? Anaweza kuchukua kitu kilichotokana na uumbaji wa asili, na kukipotosha kutoka kwenye msimamo wake wa asili, ili kutengeneza kitu kikuu, lakini hawezi kuumba. Ni Mungu pekee anayeweza kuumba, Yeye pekee.

69 Nasi tunaona katika hili, basi, ya kwamba, Shetani akikichagua kichwa cha mwanadamu, alichukua sehemu yake ya kiakili. Na sasa kanisa limeanza kutembea katika sehemu za kiakili za mwanadamu. "Loo, ni kanisa kuu. Tuna dhehebu kubwa. Sisi ndio wa kale zaidi nchini." Lakini, ndugu, mpaka huyo mwanamume au mwanamke, au mvulana au msichana, ameongoka kabisa, atazichukua dhana za kiakili, na kusema, "Biblia haimaanishi *Hili*, wala haimaanishi *Lile*. Siku za miujiza zimepita. Na hakuna kitu kama mambo haya mengine. Hapo, *Hiyo*, Hiyo si kweli," unasema, "na hizo siku zimepita." Kwa sababu analitazama kiakili.

70 Lakini hebu mtu yuyo huyo achukue maarifa kidogo aliyo nayo kichwani mwake, na kumkabidhi Mungu, na hebu Roho wa Mungu aliye hai ashuke ndani ya moyo wake, ataita kila Neno la Mungu, "Kweli," na kila ahadi, "ya Kiungu." Ndipo anaweza kufanikisha kwa ajili ya Mungu.

71 Mnaona, sehemu hiyo ndogo, chumba kidogo ndani ya moyo wa mwanadamu, Mungu alitengeneza hicho hapo ndani kwa ajili yake Mwenyewe. Hicho ndicho chumba Chake cha kudhibitia. Anaketi humo kukudhibiti. Hapo ni mahali Pake. Humo ndimo anapotumia ujumbe Wake, chumba cha kudhibitia.

72 Anawezaje kufanya kazi na wewe wakati asili ya roho ya ibilisi iko humo ndani? "Na kila mtu aliyezaliwa duniani amezaliwa katika dhambi, akaumbika katika uovu, akaja ulimwenguni akisema uongo." Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, katika asili hiyo ya kimwili, ya Adamu, mtu anawezaje kufanikisha chochote, kwa kupitia tu usomi wake?

73 Lakini atakapofikia kuwa kiumbe kipya, na utu wa kale umekufa, naye Mtu huyo mpya, Kristo, anachukua kiti Chake cha enzi ndani ya moyo wa mwanadamu, basi maisha yanaonekana tofauti, ndipo anaanza kupitia njia mpya. Kutoka kwa nia zake za ubinafsi, hadi, mawazo makubwa ya kujifanya kuwa kitu kikubwa, anaanza moja kwa moja kuelekea Kalvari, kumtambua Mungu. Kisha yake yote, lengo lake, nia yake, mafanikio yake, na yote aliyo, yanatulia katika utukufu wa msalaba, ambapo Kristo alilipa gharama kwa ajili ya maisha ya mwanadamu. Kristo ndiye Uzima wetu.

74 Ndiyo maana Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi hata kuuelewa Ufalme wa Mungu." Huwezi kuuelewa. Haiko ndani yako kuuelewa.

75 Basi kwa nini Mungu aliandaa mahali hapo padogo? Alipaandaa ili uweze kujazwa humo ndani. Huna budi kujazwa na kitu fulani. Huwezi kuwa mwanadamu, bila kujazwa. Wakati umewadia ambapo unalazimika kufanya uamuzi, na huo ni sasa, kwa sababu inalazimishwa duniani kote.

76 Nimewasikia wahudumu wakiinuka na chati na kujaribu kueleza alama ya mnyama ilikuwa ni nini. Lakini, aina fulani ya chati, haihitaji chati. Maandiko yanasema, "Wote ambao hawakupokea Muhuri wa Mungu walikuwa na alama ya mnyama." Kuna matabaka mawili tu duniani. Moja lina Alama ya Mungu, hilo jingine lina alama ya ibilisi. Na wote ambao hawakupokea Alama ya Mungu walikuwa na alama ya ibilisi. Hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema.

77 Kwa hivyo, unalazimika kufanya uamuzi. Na hebu nilishindilie ndani yenu, sio kuwa mkorofi au—au mbaya, bali kuwaambia Kweli na kuwaonya. Mwanadamu hana budi kufanya jambo juu yake. Ni ninii yako . . . Inalazimishwa kwako. Inakubidi kufanya uamuzi.

78 Ndipo kama ninaweza kuwaonyesha, kwa Neno la Mungu, Muhuri wa Mungu aliye hai ni nini, basi mtajua. Biblia ilisema, katika Waefeso 4:30, mara moja, mahali pengi kote katika Maandiko, ya kwamba Roho Mtakatifu ndiye Muhuri wa Mungu. Basi, bila Roho Mtakatifu, umetiwa alama upande ule mwingine; haijalishi una akili kiasi gani, wewe ni mshiriki wa madhehebu mangapi makubwa, jinsi ulivyo mtauwa na wa kidini.

79 Shetani alikuwa ni kitu kile kile. Shetani si mnyama mkubwa mwenye mkia uliogawanyika na kwato zilizogawanyika. Yeye ni roho. Nayo Biblia ilisema, "Mjanja sana hata angewadanganya walio Wateule kama yamkini." Yeye ni wa kidini.

80 Hivi Kaini hakuwa mtu wa kidini tu kama Habili alivyokuwa? Hivi Kaini hakutoa sadaka kama vile Habili alivyotoa? Hivi Kaini hakumjengea Bwana kanisa, kama vile Habili alivyofanya? Hivi Kaini hakushuka na kuabudu vile vile tu kama Habili alivyofanya? Hivi Kaini hakutoa dhabihu sawa sawa na Habili? Lakini mmoja alikuja kwa dhana ya kiakili, akaleta maua na matunda ya kondeni, na kuyapamba madhabahu yake, ya kiakili.

81 Lakini Habili, kwa imani, alichagua mwana-kondoo, kwa kuwa ilikuwa damu na uhai zilizohitajika, naye akamkokota kwenye jiwe na kupiga maskini koo lake dogo mpaka akavuja damu hata kufa. Mungu alisema, "Huyo ni Habili mwenye haki." Hiyo ni kweli. Ilimjia namna gani? Kwa ufunuo, si kwa kiakili. Kupitia moyo wake alijua hilo.

82 Yesu alisema, "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayatalishinda." Ufunuo wa kiroho, dhana ya kiroho! "Mwanadamu hutazama nje," Maandiko yanasema, "Mungu huangalia moyo."

83 Umejazwa na kitu. Unaweza kuwa umejazwa na mashaka. Maskini mioyo yenu inaweza kuwa imejaa mashaka. Natumaini sivyo. Mioyo yenu inaweza kuwa imejaa wasiwasi na masumbuko. Na huenda ikawa kwamba mioyo yenu imejaa matatizo.

84 Na huenda ikawa kwamba mmejawa dini, akili, theolojia nzuri iliyotiwa manukato, mkiwa wafuasi wa yale makanisa makubwa ambayo yamekuwepo kwa miaka mingi, mkiketi nyuma kwa ujasiri mwezavyo kuwa. Ndugu, hebu nikwambie, unaweza kuleta washiriki kwenye kanisa hilo hadi utakapozeeka na kufa, wala hutafanya lolote ila kujenga mnara mwingine wa kwenda Babeli. Bila shaka!

85 Unaweza kuwa umejaa upumbavu, unaweza kujaa upuuzi, unaweza kujaa chochote, lakini huwezi kubaki mtupu! Biblia inasema huwezi.

86 Biblia ilisema, "Pepo mchafu anapomtoka mtu, hutembea mahali pasipo na maji, akitafuta mahali pa kupumzikia. Kisha

anarudi na pepo wengine saba wabaya kuliko alivyokuwa, basi hali ya mwisho ya mtu huyo ni mbaya mara nane kuliko ilivyokuwa mwanzoni."

87 Ndivyo inavyofanyika kwa mikutano hii, wakati watu wanapoenda katika miamsho nao hao watu wanaongozwa tu kwa dhana ya kiakili. Anaenda zake na kujiunga na kanisa fulani, na kuacha mambo yaendelee hivyo, akiwa ameridhika. "Hiyo ni sawa. Hakuna kitu kwa upuuzi huu mwingine wote. Hatupaswi kuwa Nao." Mchungaji anasema, "Loo, ni hayo tu. Hiyo ilikuwa huko nyuma sana katika wakati mwingine." Na muda si muda mwajua, huyo ibilisi anarudi na pepo wengine saba, naye anakuwa ibilisi wa kidini. Kisha amejaa kweli kweli. Kisha ana kiburi na wivu. Na—na yeye—yeye—yeye hata amemkasirikia Mungu yeye yule aliyeiandika Biblia, anatazama kule chini, na kusema, "'Mambo haya nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya.' Hiyo ilikuwa kwa ajili ya mwanafunzi."

88 "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili," alisema Yesu, agizo Lake la mwisho kwa kanisa. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Umbali gani? "Ulimwenguni kote." Kwa akina nani? "Kila kiumbe." Ati ishara hizi zitafuatana na *baadhi* yao? Maandiko yanasema, "Zitafuatana na hao," wote, "wanaoamini. Katika Jina Langu watatoa pepo. Watanena kwa lugha mpya. Wakishika nyoka au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hivyo ndivyo Yesu alivyosema.

89 "Ishara hizi zitafuatana na waaminio," si wenye fikra hasi, si wafuasi wa kanisa wenye akili; bali waaminio waliozaliwa mara ya pili ambao wametoka kwa akili, hadi moyoni, ambapo Mungu anaketi kwenye kiti cha enzi katika chumba Chake cha kudhibitia, kudhibiti mihemko yako, kudhibiti imani yako, kudhibiti tabia yako.

90 Mungu anataka kukujaza. Kwa nini anataka kukujaza? Anataka kukujaza na nini? Anataka kukujaza na Yeye Mwenyewe, Roho Mtakatifu, kujazwa na Roho Mtakatifu!

91 Yesu alisema, katika Luka 24:49, ya kwamba, "Mtapokea nguvu, akisha kuwajilia juu yenu huyu Roho Mtakatifu. Ndipo mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, Uyahudi, na Samaria, hata miisho ya dunia." Lini? Wakati umepokea digrii yako ya udaktari? Ukiisha kuona umepokea Shahada ya Sanaa? Hapana. "Lakini mkiisha kumpokea Roho Mtakatifu, ndipo mtakuwa mashahidi Wangu katika kizazi hiki, vizazi vijavyo, hata miisho ya dunia."

92 Na katika Siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu alipokuja kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, akaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi, ishara na maajabu yalifanyika kati yao.

93 Nao wasomi wakasema, "Wanaume na ndugu, tufanye nini tupate kuokolewa?"

94 Petro akasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina lake Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

95 Huyo Ndiye Mungu anataka ujazwe naye. Anakutaka ujazwe na Roho Mtakatifu, na ndipo utaunganishwa. Na nini, kanisa? Hapana, bwana. Utaunganishwa. Na kitu gani, kanuni ya imani? Hapana, bwana. Utaunganishwa na Mungu. Nawe na Yeye mtakuwa mmoja, kama Yeye na Baba walivyo mmoja. Na Roho Mtakatifu wa Mungu ataishi ndani yako. Na kazi zile zile alizozifanya Roho Mtakatifu alipokuwa hapa ndani ya Kristo Yesu, zitafanywa ndani yako, kwa maana Yeye alisema angezifanya. Kisha sisi ni mmoja.

96 Yesu aliombea jambo hilo, katika maombi usiku wa leo, Bwana wetu wa Mbinguni aliomba kwa Baba, kwamba tuwe "mmoja" kama Yeye na Mungu walivyo mmoja. Nao walikuwa karibu kiasi gani? Mungu alikuwa ndiye Uzima na Roho ndani Yake! Na tukiwa mmoja pamoja Naye, tutakuwa, Uzima na Roho Wake utakuwa ndani yetu. Ndipo, dhana ya kidunia, ya wenye akili wa kimwili, na kanuni za imani na mafundisho ya sharti, yatatoweka; ndipo ujuzi mpya, usioghoshiwa, uliofanyizwa, wa kuzaliwa mara ya pili, wa ubatizo wa Roho Mtakatifu utafanyika katika moyo wa mwanadamu. Ndipo mtakuwa mmoja, ndipo ndugu atakuwa ndugu kweli, dada atakuwa dada. Malengo yako na nia zako, na yote uliyo, na yote utakayo kuwa, au unayojaribu kuwa, yatakuwa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu; haijalishi unawakilisha kanisa gani, uendako, au ufanyacho.

97 Kuna watu wengi sana siku hizi wanaosema, kwamba, "Roho Mtakatifu si halisi siku hizi."

98 Wakati makumi ya maelfu yao, na mamilioni, wanasema sivyo, kuna wengi hivyo wanaofurahia baraka Zake. Sana sana ni watu maskini, watu ambao wamevunjwa moyo na kukataliwa na ulimwengu, watu ambao wametupwa nje ya makanisa kwa sababu waliamini kwamba Mungu ni Mungu, lakini wamejazwa na Roho Wake. Wana kusudi moja. Wao ni kitu kimoja moyoni. Watu hao ni akina nani? Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Katoliki, Shahidi wa Yehova, Orthodoksi, Myahudi, wote pamoja, wanakuwa kitu kimoja. Si *mmoja*, kwa kanuni ya imani; si *mmoja*, kwa dhehebu; hiyo ni kazi ya ibilisi, kupitia dhana za kiakili.

99 Lakini, matendo ya Roho Mtakatifu, Ufalme wa Mungu ndani yako! Mungu huketi juu ya kiti cha enzi cha moyo wako, katika chumba Chake cha kudhibitia, akidhibiti hisia zako, na kudhibiti nguvu zako, akidhibiti dhana zako, na

kukufanya kuwa kitu kimoja na Yeye, katika ushirika na katika upendo. Naye Mungu anakujaza upendo. Anakujaza nguvu. Anakujaza Roho. Anakujaza asili Yake Mwenyewe ya Kiungu, Naye anabadilisha asili yako ya kimwili kuwa asili Yake. Kisha, katika hili, unakuwa kiumbe kipya katika Kristo.

100 Kisha, ule upendo! Unatoka nje, inaonekana ndege wanaimba tofauti. Loo, ni tofauti jinsi gani Kristo ajapo! Jinsi unaweza kuangalia nyuma na kuwazia, "Nilipataje kukaa mbali Nalo? Je, nilipataje kulikataa?" Kila kitu ni tofauti. Huna adui; wote wanaonekana watamu. Unaweza kusamehe kila kitu ambacho kimewahi kufanywa. Adui mbaya kuliko wote, ungeweza kumwombea barabarani, umkumbatie na kumwinua; haidhuru ni wa kanuni gani ya imani, yeye ni mfuasi wa dhehebu gani, yeye ni kiumbe ambaye Kristo alimfia. Huyo Ndiye Mungu anataka ujazwe naye. Huko ndiko kujaza. Huo ndio Ufalme. Hicho ndicho tulicho kitu kimoja ndani yake.

101 Sisi ni kitu kimoja, basi, sio—si kuendeleza dhehebu, si kuendeleza dini fulani potovu au—au kanuni fulani ya imani. Sisi ni kitu kimoja, kuuendeleza Ufalme wa Mungu. Ndipo tunachukua Ramani Yake, na, kila wakati Biblia iliyobarikiwa inaposema jambo lolote, Roho Mtakatifu ndani yako anapaza sauti, "Ni kweli! Ni Neno Langu!"

102 Yeye hasemi, "Je, daktari Jones alisema? Vipi kuhusu *hili*? Au, je, Daktari *Nanii*?" Haileti tofauti yoyote aliyosema daktari.

103 Yesu alisema ni Kweli. "Na mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitapita kamwe." Hapo ndipo tunapokuwa kitu kimoja.

104 Ninyi nyote, Methodisti, Wabaptisti, Presbiteri, ambao nyote. . . Hata uwe nani, sisi ni kitu kimoja. Usiruhusu shetani atumie jicho lako. Acha Mungu autumie moyo wako. Ukiangalia na kujaribu kuelewa ni nini, ni nini kinacholifanya, "Inatokeaje namna hiyo?" Hulitilii Hilo swali unapompokea Roho Mtakatifu. Ikiwa bado unatilia shaka Neno la Mungu, inaonyesha kwamba Mungu hayuko moyoni mwako. Roho Mtakatifu hahoji jambo moja ambalo Mungu anasema. Anasema, "Amina na amina! Ni kweli, maana Mungu alisema hivyo!" [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

105 Ibrahimu aliviita vile vitu ambavyo havikuwepo, kana kwamba vilikuwapo, kwa sababu Mungu alisema hivyo. Mungu alimwambia, akiwa na umri wa miaka sabini na mitano, na Sara akiwa na sitini na mitano, wangepata mtoto. Mbona, ilikuwa ni ujinga, kufikiria hivyo. Lakini, Mungu alisema hivyo, na Ibrahimu alikuwa mwana wa Mungu. Naye alitembea miaka ishirini na mitano, akiita kila kitu . . .

Kila siku, "Sara," angesema, "Ukoje, mpendwa?"

106 "Sihisi tofauti yoyote kuliko nilivyowahi kuhisi." Alikuwa amekata hedhi kwa muda wa miaka arobaini. Kamwe hakupata

watoto, alipokuwa akiishi naye, alipokuwa na umri wa miaka kumi na saba. Lakini alimwamini Mungu, na kuita kila kitu kilicho kinyume chake kana kwamba hakikuwa, naye akaliita Neno la Mungu kuwa ni Kweli.

Mwezi wa kwanza ukapita. "Unajisikiaje, Sara?"

"Hakuna tofauti."

"Vema," anasema, "Mungu asifiwe, tutapata mtoto hata hivyo!"

Mwaka ukapita. "Unajisikiaje?"

"Hakuna tofauti."

"Lakini tutampata, kwa vyovyote vile!"

107 Nayo Biblia ilisema, "Badala ya kuwa dhaifu, alizidi kupata nguvu wakati wote." Ingekuwa muujiza zaidi. Mungu alisema hivyo, haina budi kutukia.

108 Miaka ishirini na mitano, na sasa ana miaka tisini, naye mia moja. Siku moja Malaika alishuka, mgongo Wake ulikuwa umeelekezwa kwenye hema, Naye akasema, "Ibrahimu, nitakuzuru," Naye akamwambia Ibrahimu yale yatakayotukia.

109 Ndipo mtoto Isaka akazaliwa. Kwa nini? "Kwa sababu Ibrahimu hakusita katika ahadi ya Mungu, kwa kutokuamini, bali alikuwa na nguvu, akimsifu Mungu." Kwa nini? Haikuwa akilini mwake; ilikuwa moyoni mwake.

110 Kiti cha enzi cha Mungu kiko ndani ya moyo wa mwanadamu. Hapo tunakuwa mmoja, mmoja katika kusudi, mmoja katika mafanikio. Kama ndugu Mmethodisti akiwaleta watu mia moja kwa Mungu, "Amina na amina!" Kama Mpresbiteri, yeyote yule, akiwaleta watu kwa Kristo, "Amina na amina!" Kama Tommy Osborn akiwaleta watu milioni moja mwaka huu, na Oral Roberts watu milioni moja, na Billy Graham watu milioni moja, na kila dhehebu lingine watu milioni moja, ninaweza kusimama na kumsifu Mungu aliye hai. Kwa sababu, huo ndio tunaofanikisha, Ufalme wa Mungu, hilo ndilo lililo lengo letu kufanya, kupeleka watu Kwake. Wao ni Wakristo waliozaliwa mara ya pili. Hapo ndipo tunapokuwa kitu kimoja. Tumeungana pamoja. Sisi ni ndugu.

111 Na sio maadamu, mnasema, "Vema, wao si Wamethodisti. Wao si Wabaptisti. Wao si *hiki, kile*, au *kinginecho*." Basi nia ya—yako yote si sahihi, na lengo lako, na yote unayofanikisha si mazuri; unapojaribu kufanya kitu ndani yako, ili uonekane mkubwa, huku wewe ni mdogo. Kumbuka.

112 Je, uliwahi kuona ngano ikikua? Ukiona ngano ikisimama na kujitikisa tu namna *hiyo*, kumbuka, hakuna kichwa ndani yake. Ni tupu. Kichwa kilichojaa huinama kila wakati. Naye mtu aliyejaa, na amejawa na wema wa Mungu na rehema Zake,

huinamisha kichwa chake kwa unyenyekevu. "Atakayejidhili, Mungu atamkweza. Ajikwezaye atadhiliwa."

113 Marafiki, wakati umewadia kwa wanaume na wanawake kutambua ukweli kwamba tunataka kuwa kitu kimoja. Yesu aliomba kwamba tuwe kitu kimoja, kama vile Yeye na Mungu walivyokuwa mmoja. Naye Mungu alikuwa ndani Yake. Nasi ni mmoja pamoja na Kristo tukimruhusu Kristo aingie. Lakini ndiyo njia pekee tunayoweza kufanya, ni kumwacha Yeye achukue chumba cha udhibiti mioyoni mwetu, ndipo tunakuwa kitu kimoja.

114 Tunakabiliwa na Krismasi. Tunakabiliwa na wakati. Tunakabiliwa na mambo ya kutisha. Haya yote tunayokabiliana nayo, yanaleta tofauti gani, ni nini kijacho au kiendacho, maadamu Kristo yuko ndani ya chumba cha kudhibitia, akitutawala, akitutawala na kutupa imani ya kuamini mambo ambayo hatuwezi kuyaona? Mungu alisema sisi . . .

115 "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana." Unaamini, kwa maana Mungu yuko moyoni mwako, na kukwambia ya kwamba Neno Lake ni kweli. Wala hakuna Roho atakaye, wa Mungu, atakayekana Neno lolote la Mungu. Roho wa Mungu atawatambua Walio Wake. Loo, jinsi nilivyo na furaha, kujua kwamba kuna Mungu, kwamba Yeye ni halisi.

116 Siku moja kulikuwa na ninii . . . hapa juu Indiana, kulikuwa na wavulana wawili waliolelewa huko nje mashambani. Nao walikuwa maskini hohehahe, wavulana wakulima. Nao walikua pamoja. Basi, siku moja, mmoja wao akaoa. Siku chache baadaye, yule mwingine akaoa.

117 Ndipo mmoja wao akaenda mjini, kuishi. Naye alikuwa ameanza kucheza soko la hisa, akaachana na Mafundisho yake ya utotoni, akaingia kwenye jambo baya. Basi akazicheza, naye akatajirika zaidi na zaidi, hata hatimaye akawa milionea mkubwa. Kisha akahamia Chicago, na kuingia kwenye mojawapo ya barabara kuu na kujijengea jumba la kifalme. Yeye na mkewe walikimbilia vilabu vya usiku, nao wakanywa kokteli, kisha wakalala nje, usiku kucha. Walikuwa na wanyweshaji na kila kitu, kuwapa chochote walichotaka. Nao walidhani walikuwa wanaishi kweli.

118 Lakini mtu anayeishi hivyo hana amani. Hakuna amani kwa moyo unaosumbuka. Kwa moyo wenye dhambi, hakuwezi kuwa na amani. Kama mtu anatamani kunywa pombe, na anaita huko "maisha," anadhani ana wakati mzuri sana, inaonyesha utupu wake. Hebu mchukue mtu, atengeneze dola milioni moja, anataka mbili. Mchukue mtu anayeenda kwenye karamu na kunywa kinywaji kimoja, usiku wa leo, anataka kingine. Mchukue mwanamume, asiwe mwaminifu kwa mkewe, mara moja, atafanya hilo tena; na vinginevyo. Unaona, ni kitu fulani,

na hakuridhika kamwe. Anaweza kuwa na dola milioni moja mkononi mwake, ama milioni kumi mkononi mwake; analala usiku, na mtokoso wa ulevi juu yake; anaamka, kesho yake asubuhi, anasumbuka, jinamizi, akili zimetatizika. Ati mnaita hiyo amani? Hiyo siyo amani.

119 Lakini mtu anaweza kukosa hata mto wa kuwekelea kichwa chake, anaweza hata asimiliki jozi moja ya viatu maridadi, au kuweza kuwa na chakula kizuri nyumbani mwake; lakini endapo Mungu anatawala moyoni mwake, analala kwa furaha na kuamka kwa furaha. Ni amani ya kudumu. Ni jambo ambalo Mungu hufanya.

120 Huyu jamaa alikuwa amesahau Mafundisho hayo. Alikwenda kucheza kamari. Wakati wa Krismasi ukawadia. Akawazia juu ya rafiki msiri wake, kwa hiyo akamwandikia barua. Mmoja wao aliitwa Jim, yule tajiri, na John ndiye aliyekuwa maskini. Naye akamwandikia barua, akasema, "John, laiti ungelikuja kuniona, wakati wa likizo. Ningependa kukutana nawe, kuzungumza nawe tena. Sijakuona kwa miaka mingi."

121 Akamjibu, akasema, "Ningependa kuja, Jim, lakini siwezi kuja. Sina pesa, za kuja."

122 Cheki ikaja kwa barua, katika siku chache, ilisema, "Haya njoo! Nataka uje, kwa vyovyote vile." Kwa hivyo John akajitayarisha, kijana wa mashambani, akavaa jozi safi ya ovaroli, na kofia yake ya makuti, na—na kanzu ndogo ya rangi tofauti, kisha akapanda treni.

123 Basi alipofika kule, kulikuwa na dereva ameketi pale, kumlaki, akiwa na limuzini kubwa. Hakujua jinsi ya kutenda. Aliingia kwenye limuzini hii, akiwa ameshikilia kofia yake mkononi, akitazama pande zote. Wakafika kwenye jumba kubwa mno la kifalme, huko Chicago.

124 Akatoka akaelekea mlangoni, na kubonyeza kengele. Ndipo mnyweshaji akatokea, kasema, "Kadi yako, tafadhali, bwana." Hakujua alichokuwa akizungumzia. Akampa kofia yake. Alikuwa. . .Hakujua chochote kuhusu kadi ya mapokezi. Hakuwa na mengi ya mali ya ulimwengu huu. Akasema, "Nataka kadi yako."

125 Akasema, "Sijui unachozungumzia, bwana." Kasema, "Jim aliagizia nije. Hayo ndiyo yote nijuayo."

126 Kwa hiyo akarudi na kumwambia mwenzake, ambaye alikuwa bado hajaamka kitandani. Akasema, "Kuna mtu wa ajabu-ajabu amesimama mlangoni." Kasema, "Amevaa. . . Sijawahi kuona mtu aliyevalia kama yeye. Naye alisema Jim alimwalika."

Akasema, "Mwambie, 'Karibu ndani.'"

127 Akajizungushia nguo ya kushindia nyumbani, akashuka ukumbini akukutana na maskini rafiki yake huyu wa mashambani, na kumpa mkono. Kasema, "John, hujui jinsi ninavyofurahi kukuona!"

128 Naye maskini yule jamaa wa mashambani amesimama, akitazama huku na huku chumbani, akasema, "Jim, hakika unayo mengi."

129 Akasema, "Ninataka kukuonyesha kote." Akampeleka juu ghorofani, na nje kwenye baraza la kuotea jua, akafungua dirisha.

Kasema, "Martha yuko wapi?"

"Loo," kasema, "bado hajaingia. Alitoka, jana usiku."

Kasema, "Uh, mnaendeleaje nyote?"

130 Kasema, "Loo, si sana. John, wewe na Katie mnaendanaje?"

Kasema, "Vizuri tu."

Kasema, "Loo, yuko nyumbani?"

131 Kasema, "Naam, tuna watoto saba." Kasema, "Nyinyi mna watoto wowote?"

132 Kasema, "Hapana, Martha hakutaka kuwa na yeyote." Kasema, "Aliona afadhali tusiwe na watoto wowote; inaingilia maisha ya kijamii. Wajua," akainua mapazia, akasema, "angalia hapa." Kasema, "Unaiona benki ile huko ng'ambo?"

Akasema, "Naam."

133 Kasema, "Mimi ndiye rais katika benki hiyo." Kasema, "Unaiona hiyo kampuni ya reli?"

"Naam."

Kasema, "Nina hisa zenye thamani ya dola milioni moja huko."

134 Naye akatazama kule chini, na akaona zile bustani kubwa, na kila kitu, jinsi zilivyoonekana za kupendeza. Basi maskini John akasimama pale na kofia yake ya makuti mkononi, akitazama huku na huku. Akasema, "Hilo ni jema, Jim. Hakika ninashukuru kwamba umefanikiwa." Kasema, "Mimi na Katie hatuna mengi." Kasema, "Bado tunaishi katika ile nyumba ndogo ya kale iliyoezekwa kwa viezekeo chini kule." Kisha kasema, "Hatuna mengi sana, lakini tuna furaha tele."

135 Papo hapo kundi la waimbaji wa nyimbo za Krismasi, sauti zao zikaanza kuingia:

> Usiku mtulivu, usiku mtakatifu!
> Yote ni shwari, na yote ni angavu.
> Kumzunguka mama bikira mchanga pamoja na Mtoto.
> Mtoto mchanga mtakatifu mpole sana na mpendwa.

136 Jim akageuka na kumtazama John; John akamtazama Jim. Kasema, "John, nataka kukuuliza jambo fulani." Kasema, "Unakumbuka tulipokuwa wavulana? Nasi tulikuwa tukienda kwenye lile kanisa dogo jekundu la kale pale kando ya barabara, na tungesikia hao wanakwaya wa kale wa mashambani wakiimba nyimbo hizo?"

Kasema, "Naam."

Kasema, "Bado unaenda huko chini?"

137 Kasema, "Naam, bado niko huko." Kasema, "Mimi ni shemasi huko chini sasa." Kasema, "Na wewe je, Jim?" Kasema, "Ulikuwa unazungumza kuhusu kiasi unachomiliki hapa chini." Kasema "Unamiliki kiasi gani *Huku* juu?"

138 "John, samahani," kasema, "similiki chochote Huko juu." Kasema, "Kumbuka, kabla tu ya Krismasi mwaka mmoja, hatukuwa na viatu?" Kisha kasema, "Tulikuwa na hamu zaidi ya kununua baadhi ya fataki kwa ajili ya Krismasi." Kisha kasema, "Tulitoka huko nje na kuweka mitego ya masanduku, kuwanasa sungura, kununulia fataki kwa ajili ya Krismasi." Kasema, "Unakumbuka asubuhi ile sungura yule mkubwa wa mwituni alikuwa kwenye ule mtego wako wa sanduku?"

John akasema, "Naam, nakumbuka."

139 "Ungenunua fataki kadhaa. Nawe ulienda na ukanunua kadhaa, ukanigawia."

Akasema, "Naam."

140 Kasema, "John, nitagawanya chochote nilicho nacho, pamoja nawe. Lakini kitu kimoja natamani ungenigawia." Kasema, "Ningetoa kila kitu nilicho nacho, kama ningeweza kutembea kwenye barabara hiyo ndogo ya mavumbi, bila viatu, hadi kwenye kanisa lile dogo la kale tena, na kuhisi Uwepo huo wa Mungu aliye hai, wakati kwaya hiyo ilikuwa ikiimba, maskini yule mhubiri wa mtindo wa kale wa mashambani alikuwa akihubiri." Kasema, "Ningetoa chochote. Ningetoa yote niliyo nayo, kila hisa katika reli, na hazina zote za benki, na nyumba hii, na yote, kama ningeweza kurejea tena na kuwa na ile amani iliyobarikiwa niliyokuwa nayo nilipoipitia barabara hiyo ya kale."

141 Maskini John akachukua, akamkumbatia kwa mikono yake. Akasema, "Kulikuwa na mamajusi watatu, matajiri ambao walikuja na kuweka yote miguuni pa Yesu wakati mmoja, kama Mtoto mchanga," na kusema, "walipata msamaha wa dhambi zao." Akasema, "Ningeninii, ingawa ningeninii... Nafikiri kwamba wewe ni wa ajabu sana, Jim, katika yale ambayo umebarikiwa kufanya, mambo haya yote. Lakini afadhali niwe na mke wangu na watoto saba, wakiishi kule chini wakiwa na magodoro ya manyasi, ya kulalia, kisha niwe na

amani iliyo moyoni mwangu, kuliko kuwa na utajiri wako wote, Jim, ambao ungeweza kuwa nao."

142 Na hiyo ni kweli, marafiki. Utajiri haupimwi kwa dola. Utajiri haupimwi kwa majina makubwa na umaarufu. Utajiri ni wakati Ufalme wa Mungu unapoingia ndani ya moyo wa mwanadamu, ukabadilisha hisia zake na kumfanya kiumbe kipya katika Kristo Yesu, na kumpa Uzima wa Milele. Hicho ndicho kitu tajiri kuliko vyote duniani.

Na tuombe.

143 Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa. Je, wewe ni maskini, usiku wa leo, katika mali ya ulimwengu huu? Hata hujui jinsi utakavyolipa bili ya makaa ya mawe au bili ya mafuta, au chochote kile? Unaweza kuwa hivyo; natumai sivyo ulivyo. Lakini kama ni hivyo, kwamba uko hivyo, unaweza kuondoka kwenye jengo hili, usiku wa leo, maskini aliye na furaha kuliko wote duniani. Unaweza kuishi hapa na . . . kuondoka hapa, usiku wa leo, na mali ambayo hakuna pesa zingeweza kununua. Unaweza kuunganisha moyo wako na Kristo Yesu, Naye anaweza kuingia ndani ya nafsi yako na kuchukua chumba cha kudhibitia. Na haijalishi kijacho wala kiendacho, utakuwa na furaha siku zako zote. Hivi . . .

144 Ndiyo zawadi kubwa kuliko zote ambayo imewahi kutolewa. Loo, bila shaka, unawapa marafiki zako zawadi za Krismasi. Hilo ni jema. Hiyo ni ishara. Lakini, ndugu, kuna Zawadi iliyotolewa kwa ajili yako, usiku wa leo, ambayo hakuna pesa ingeweza kuinunua. Ni zawadi ya bure kutoka kwa Mungu: Mwanawe wa pekee, Yesu Kristo. Je, waweza kumpokea kama Kiongozi wako binafsi, kama Mwokozi wako binafsi, kama Mungu wako, kama Mkombozi wa—wako, kama Mfalme wako? Anaponya nafsi na mwili. Anachukua chumba cha kudhibitia. Ikiwa una hofu na mashaka, acha yaondoke tu sasa. Acha Yeye awe Mfalme. Acha aingie na kuchukua mamlaka. Mwache awe Bwana. *Bwana* ni "Mtawala." *Ubwana* ni "utawala."

145 Unasema, "Loo, na—naamini. Nilimfungulia Yeye moyo wangu, miaka mingi iliyopita."

146 Lakini je, amewahi kuwa Bwana wako, mwenye kudhibiti kabisa, kudhibiti hisia zako, imani yako na yote? Unaposoma Biblia, kila Neno Lake ni Kweli. Wakati amani . . . Wakati misukosuko inapokuja, una amani moyoni mwako. Ukijua kama bomu la atomiki likiitapanya dunia hii vipande vipande, usiku wa leo, ungekusanywa katika Kristo Yesu, Utukufuni, kabla majivu hayajatulia duniani. Una faraja hiyo? Kama huna, na ungependa kuwa nayo, tafadhali inua mkono wako haraka na kimya, na, kwa kufanya hivyo, useme, "Bwana, unirehemu. Sasa nataka kuunganishwa pamoja Nawe, kama mmoja wa watoto Wako katika Ufalme wa Mungu, katika nia zangu, lengo langu. Unajua yote kunihusu. Nichukue, Bwana, jinsi tu nilivyo, na

unijalie kuwa Wako"? Mungu akubariki, mwanangu. Mungu akubariki, bwana. Na Mungu akubariki, na wewe. Na wewe, ndugu. Wewe, wewe, wewe hapo. Na wewe, mama. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli.

147 Ninajua wale wa mtindo wa kale, wa kanisa la Methodisti, na kadhalika, huamini katika kuja madhabahuni, na kadhalika. Hiyo ni sawa. Ndugu, huwezi kuinua mkono wako kwa Mungu, huwezi hata kupiga hatua kuelekea Huko, isipokuwa Mungu akuguse. Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba kwanza."

148 Je, hutaheshimu na kustahi kile ambacho kimekufanya uinue mkono wako? Useme, "Naam, Bwana, ninamaanisha hivyo kutoka moyoni mwangu. Na kila dhambi niliyo nayo, ninaiweka sasa juu ya madhabahu Yako. Ninajiweka wakfu Kwako, sasa hivi, Bwana, ya kwamba tangu saa hii, na kuendelea, nitakuishia. Na tabia zangu zote na dhambi zangu zote, na zote, ninaziacha papa hapa, nikiufanya mtupu moyo wangu. Wewe kuwa Mtawala wa moyo wangu. Wewe uwe Bwana wa moyo wangu. Chukua nafasi Yako ifaayo katika maisha yangu, Bwana, na unitawale."

Yamaanishe hayo sasa, tunapoomba.

149 Bwana, nimejifunza, katika Neno Lako, ya kwamba imeandikwa, kwamba, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, kwanza. Na wote alionipa Baba, watakuja Kwangu." Mwanadamu anaweza kuishi miaka kumi, miaka ishirini, hamsini, au miaka sabini na mitano, au hata zaidi, na bado hajawahi kuja. Lakini utakuja wakati ambapo Nuru itamulika njiani mwake, na hiyo ndiyo fursa. Jinsi tulivyo na shukrani kwamba bado kuna—bado kuna Mungu anayewapenda watu! Na usiku wa leo ameonyesha rehema Yake kwetu, kwa kuachilia mikono mingi kuinuliwa, kumpokea Yesu kama hii, Zawadi kuu ya Mungu ya Krismasi, ile ya Asili. Na Zawadi pekee halisi, ya kweli, ya Krismasi iliyotumwa na Mungu ni Mwanawe wa pekee, duniani. Wapokee, Bwana.

150 Itakuja siku ambayo watabonyeza mto wakifa; au kukoroma barabarani, chini ya motokaa; au labda kugugumia kooni mwao, kutokana na kuzama majini. Sijui kikomo chao kitakuwa kipi. Lakini, Bwana, ninajua jambo hili, ya kwamba Yesu alisema Maneno haya, "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi, na kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe hata milele." Ninaamini hilo kuwa Neno Lako, Bwana. Kama nikiishi ama nife, bado ni Neno Lako, kwa maana Wewe umelinena. Na mbingu zote na nchi zitapita, bali Neno Lako halitashindwa kamwe.

151 Ulisema, "Yeye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe. Nitampa Uzima wa Milele, nami nitamfufua siku ya mwisho." Ajapozama baharini, ajapoungua motoni, hata majivu yake

yakipeperushwa katika pepo nne za nchi, "Bwana Mungu atashuka kutoka Mbinguni pamoja na Sauti ya Malaika Mkuu, na parapanda ya Mungu, nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Tutanyakuliwa pamoja nao, ili kumlaki Bwana hewani, na kuwa pamoja Naye milele." Bwana Mungu, tunaamini ya kwamba hilo litatukia.

152 Na juu ya maskini hawa watu waliokataliwa duniani, ambao wamekuja hapa usiku wa leo na kuinamisha vichwa vyao kuelekea mavumbini ulikowatoa, na ambapo watarudi, ukikawia. Wameinua mikono yao, mikono yao Kwako, na kusema, "Bwana, nimekosea. Nipokee." Loo, ungewezaje kumkataa mmoja? Huwezi, huwezi kufanya hivyo, Bwana. Ikiwa walimaanisha hivyo kutoka ndani ya moyo wao, usingeweza kufanya hivyo, na ubaki kuwa Mungu, kwa sababu wamekuja kwa uaminifu. Wao ni zawadi ya upendo ambayo Baba anakupa.

153 Sasa, kama mtumishi Wako, ninawaamuru waje Kwako; na kuzikabidhi nafsi zao, na miili yao, na roho zao, Kwako. Washike katika ulinzi Wako uliobarikiwa, Bwana. Ondoa uovu wote kutoka kwao. Ondoa dhambi, ondoa hizo tabia. Jalia zisiwasumbue kamwe, tangu usiku huu na kuendelea. Jalia watoke hapa, watu huru, wakiwa na Mungu moyoni mwao, kwenye chumba cha kudhibitia. Na adui atakapowajaribu, jalia wakumbuke Mungu yuko katika chumba cha kudhibitia, Naye Ndiye anayegeuza vichwa vyao kutoka kwa adui.

154 Nasi tutausimamisha Ufalme Wako, Bwana. "Ufalme Wako na uje. Mapenzi yako yafanyike duniani, kama huko mbinguni. Na usitutie majaribuni, Bwana, bali utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa Ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu, milele." Amina.

155 Ndivyo ilivyo imeandikwa, basi na ifanyike. Kila mtu walioinua mkono wao na kuamini kwamba Bwana Yesu Kristo, ukimkubali kama Mwokozi wako, mpokee, kutoka moyoni mwako, kwa imani. Sio kile macho yako yanachokwambia, kile akili yako inachowazia, wewe, "Siwezi kuiacha. Siwezi kulifanya. Siwezi kuacha kufanya *hivi*," hiyo ni ya kiakili. Lakini Kitu fulani huko ndani ya moyo wako, kinasema, "Nawe ni mali yangu." Kumbukeni, sikiliza kile Sauti yako moyoni inachosema, maana ni Mungu akizungumza nawe. Mambo mengine yote yatafifia kama tu vi—vile usiku hauna budi kufifia.

156 Ni upi ulio na nguvu zaidi, usiku au mchana? Hebu jua lichomoze, uone yanayoupata usiku; unafifia tu wala hauwezi kuwako tena.

157 Na wakati—wakati Roho wa Mungu anapoingia ndani ya moyo wa mwanadamu, usomi wake wote hufifia tu, na giza na mashaka yanaondoka tu. Wala huwezi kuvipata tena, kwa sababu hakuna nafasi kwa ajili yake. Nuru imejaza nafsi yake.

Anatembea katika Nuru. Yuko kwenye Nuru. Yeye ni mtoto wa Mungu, na Mungu anampenda.

Sasa ningependa kuimba wimbo, sisi sote, pamoja.

Mimi ni mwana wa Mfalme!
Mwana wa Mfalme!
Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
Mimi ni mwana wa Mfalme!

158 Ni wangapi wanaojisikia hivyo sasa, inua mkono wako, "Mimi ni mwana wa Mfalme"? Ninyi mlioinua mikono yenu, muda mfupi uliopita, iinueni. Liaminini. Kaeni nalo. Mungu anaujua moyo wako.

159 Njoo, mchungaji, hebu. . .Siwezi kuongoza nyimbo, lakini hebu tuuimbe wimbo huo. Utanisaidia, sivyo? Ninyi nyote, pamoja sasa, vema, tunapouimba huu. Vema. Ninaamini dada yetu anakuja, pamoja na—na. . .kutupa sauti kwa muziki. Nilitazama huku na huku, sikumwona popote, na hiyo ndiyo sababu nilisema hivyo. Ni wangapi wanaoujua, "Baba yangu ni tajiri wa nyumba na mashamba, anashikilia utajiri wa dunia mkononi Mwake"? Hebu wazia tu jinsi hilo lilivyo zuri. Vema, kila mtu sasa, pamoja.

Baba ni tajiri wa nyumba na mashamba,
Yeye anashikilia mali ya ulimwengu mkononi
Mwake!
Ya yakuti na almasi, ya fedha na dhahabu,
Maghala yake yamejaa, ana mali isiyoelezeka.

160 Sasa, kimya kabisa sasa.

Mimi ni mwana wa Mfalme!
Mwana wa Mfalme!
Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
Mimi ni mwana wa Mfalme!

161 Ni ajabu hiyo? Unaamini wewe ni mwana wa Mfalme? Inua mkono wako, nyote mnaoamini kwamba ninyi ni wana wa Mfalme. Vema. Sasa tunapouimba huo tena, nataka upeane mikono na mtu nyuma yako, mtu fulani mbele yako, mtu kulia na kushoto, haijalishi ni akina nani, una imani gani, kama wewe ni mwana wa Mfalme, huku tukiuimba tena.

Mimi ni mwana wa Mfalme!
Mwana wa Mfalme!
Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
Mimi ni mwana wa Mfalme!

Hema au nyumba ndogo, kwa nini nijali?
Wananijengea jumba la kifalme Kule!
Ya yakuti na almasi, ya fedha na dhahabu,
Maghala yake yamejaa, ana mali isiyosemeka.

Mimi ni mwana wa Mfalme!
Mwana wa Mfalme!

Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
Mimi ni mwana wa Mfalme!

Kuwa kama Yesu, kuwa kama Yesu,
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maishani toka duniani
hadi Utukufuni
Naomba tu kuwa kama Yeye.

162 Je, hiyo ndiyo shauku yako? Yeye ni wa ajabu sana! Ninampenda kwa yote yaliyo ndani yangu. Nilisalimisha kila kitu nilichokuwa nacho, miaka ishirini na minane iliyopita, kwa Bwana Yesu. Tangu wakati huo, nimekuwa kwenye uwanja wa vita, nikifanya yote nijuayo, kuwaongoza wanaume na wanawake kuitazamia taji hiyo ya utukufu.

163 Ukianza kunena juu ya Kuja kwa Bwana, watu walisema . . . Mtu mmoja aliniambia, si muda mrefu uliopita, “Loo, mhubiri, usiongee namna hiyo.”

Nikasema, “Hivi wewe ni Mkristo?”

“Naam, lakini, jamani, tuna mengi ya kufanya bado.”

164 Nikasema, “Jambo la furaha zaidi ninaloweza kufikiria ni Kuja kwa Bwana.”

165 Paulo alisema, mwishoni mwa safari, “Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda. Na tangu sasa nimewekewa taji ya haki; Bwana, Hakimu mwenye haki, atakayonipa siku hiyo. Sio mimi tu, bali wale wote wanaopenda kuonekana Kwake.”

166 Ningekubadilisha na nini, inanibidi kufanya nini, kwa kuwa ninazeeka? Mwili huu mkongwe, dhaifu, unaougua ambao umejaa uharibifu, utabadilishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho. Nitakuwa kijana milele. Sitakuwa na kipindi cha magonjwa tena. Sitawahi kulia machozi. Sitazeeka kamwe, kamwe. Sitakufa kamwe. Sitakuwa mgonjwa kamwe. Sitawahi kuwa na huzuni au wasiwasi. Lakini, nitakuwa na mwili kama Mwili Wake Mwenyewe mtukufu. Ikiwa mimi . . . Ikiwa hicho si kitu cha kuishia! Ikiwa hilo silo jambo kuu ninalojua!

“Je, ninaipataje?”

167 Ni Zawadi ya bure. [Ndugu Branham anagongagonga kwenye mimbara—Mh.] Mungu anabisha, nami nasema, “Naam, Bwana, Wewe ni Muumba wangu, ninakukubali.” Ananitia muhuri ndani, kwa Roho Mtakatifu, ndani Yake, ndipo basi sioni chochote ila Yesu na Damu Yake.

Ni nini kinachoweza kuosha dhambi zangu?
Hakuna ila Damu yake Yesu;
Ni nini kinachoweza kunifanya mzima tena?
Hakuna ila Damu yake Yesu.

Loo, mtiririko huo ni wa thamani

Unaonifanya mweupe kama theluji;
Sijui chemchemi nyingine,
Ila Damu yake Yesu.

168 Je, hamna furaha? Najua hakuna kanuni ya imani inayoweza kufanya hivyo. Najua hakuna madhehebu yanayoweza kufanya hivyo. Najua hakuna kanisa linaloweza kufanya hivyo. Najua hakuna mtu anayeweza kufanya hivyo. Najua hakuna maji yanayoweza kufanya hivyo. Najua hakuna theolojia inayoweza kufanya hivyo. "Ila Damu ya Yesu!"

Matumaini yangu hayajajengwa juu ya chochote
Pungufu ya Damu ya Yesu pamoja na haki;
Wakati yote yanayoizunguka nafsi yangu yakitoweka,
Basi Yeye ndiye tumaini langu lote na nanga yangu.

Je, huyo ni wewe?

Kwa kuwa juu ya Kristo, Mwamba wenye imara, tunasimama;
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao,
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

169 Mungu awabariki sasa. Ninaamini kuna kuwekwa wakfu kwa mtoto, naamini. [Ndugu Neville anasema, "Naam."—Mh.] Kwa hiyo, kwa wakati huu, nitarudisha ibada kwa mchungaji, kwa ajili ya hii. Njoo moja kwa moja mbele, Ndugu Neville. Bwana akubariki.

58-1221E Umoja wa Mungu Mmoja Katika Lile Kanisa Moja
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org